Kama mafanikio yangekuwa ni mipango pekee basi kila mtu angekuwa nayo maradufu. Kila kitu ambacho mtu anakitamani akipate maishani mwake kingekuwa tayari kipo mikononi mwake. Kumekuwa na matamanio na mipango mbalimbali ya kupata mafanikio lakini kwa bahati mbaya watu wengi hawana mafaniko hayo.

Kama ukisema ukusanye malengo ambayo watu wanayo, utagundua kuwa watu wana malengo na mipango mizuri lakini ni mipango michache sana inayozaa matunda. Hapa kutakuwa na shida sehemu. Kwa nini watu wanajua nini cha kufanya lakini hawana matokeo?

Mwaka mpya ukifika kila mtu huwa na hamasa kubwa ya kufanya makubwa. Huu huwa ni muda wa shauku kubwa na shamra shamra huku kauli ile ya mwaka mpya na mambo mapya ikitoka midomoni mwa watu wengi. Mwaka huu lazima nifanye makubwa. Mwaka huu lazima niongeze kipato changu. Mwaka huu lazima nikuze biashara yangu. Mwaka huu lazima nisome vitabu vingi sana, mwaka huu lazima niandikie kitabu nk..

Wapo ambao huandika kabisa malengo hayo lakini wapo ambao huyafikiri tu vichwani mwao. Hamasa hizo huwafanya watu wengine watangaze nini wanachotarajia kukifanya.

Lakini baada ya muda mfupi kama miezi miwili hamasa hiyo huanza kuisha na kutowasikia wakitaja tena nini wanataka kukifanya. Baada ya shamra shamra hizo kuzima, watu hurudi kuishi maisha yao ya kawaida ya mwaka jana ambayo hayakuwa na mafanikio. Kuna shida kubwa ambayo inatenganisha mipango na mafanikio, shida hiyo ni NIDHAMU KALI.

Nidhamu ni kiungo kinachosimama kati ya malengo na matokeo. Nidhamu ndiyo inayowezesha kazi inayotakiwa mtu aifanye ile apate matokeo. Nidhamu kali ni kufanya kile ulichopanga kukifanya bila kuruhusu sababu yoyote ikuzuie. Malengo peke yake hayatoshi yanahitaji kazi ili kutoa matokeo. Mtu anapotaka kuweka kazi ili kupata matokeo, ndipo vikwazo vingi huanza kujitokeza. Vikwazo hivyo mara nyingi huambatana na maumivu.

Ili kuweza kuchukua hatua za kupata matokeo licha ya changamoto hizo unahitaji msukumo usio na ukomo, hii inaitwa ***nidhamu kali.*** Nidhamu ni kumbishia mwingine anayesema usifanye kile ulichopanga kufanya. Kwamfano umepanga kuanza kuamka mapema ili kuianza siku mapema na kwa mafanikio, muda wa kuamka ukifika, kuna mwingine anasema uendelee kulala na kwa nini ujitese! Nidhamu kali ni kumbishia huyu na kumshinda.

Kumshinda mwingine anayekubishia ni ushindi juu ya mtazamo wako. Vikwazo vyote unavyokutana navyo vinaanzia kwenye akili yako, yaani unavyochukulia jambo. Kabla ya kuomba mwili wako umshinde mwingine na huna budi kuushinda mtazamo unaoshindana na wewe.

**Nidhamu na mafanikio:** Nidhamu na mafanikio ni mapacha. Watu wamejaribu kuwatenganisha mapacha hawa lakini imeshindikana. Hii ni kwasababu hakuna mafanikio yoyote bila kuweka kazi. Lakini kufanya kazi sio zoezi rahisi kwasababu ya ugumu unaoweza kukutana nao. Nidhamu pekee ndiyo itakusaidia ujisukume uchukue hatua na kupata mafanikio.

**Kujenga nidhamu.** Nidhamu ni kitu kinachojengwa. Kuna hatua za kupitia na inahitaji muda pia ili kuwa na nidhamu yenye msimamo. Kujenga nidhamu kali ya kukuwezesha kufanya jambo lolote bila kujali maumivu au vikwazo vyovyote, si kazi rahisi ndiyo maana watu wengi hawafanikiwi. Kiungo kikuu cha kujenga nidhamu ni kujua **KWA NINI KUBWA** ya kufanya kitu hicho. Hii ni sababu ambayo itashinda nguvu ile ya kukuzuia kufanya jambo hilo. Hiki ni kitu utakachokipata kwa kujisukuma kuchukua hatua. ***Je ni kupata uhuru wa kifedha? Je ni kuwa na afya njema ya kudumu?*** Utafanikiwa kujenga nidhamu kali kama utafanikiwa kuifahamu kwa nini yako kubwa.

**Nidhamu binafsi.** Kuna aina nyingi za nidhamu ambazo mwanadamu anaweza kuzijenga lakini binafsi ndiyo nidhamu mama. Huu ni ushindi juu ya ukinzani mkubwa wa kutochukua hatua unaokutana nao ndani yako mwenyewe. Ukishaweka malengo kisha kuanza kuweka kazi, ukinzani utaanzia ndani yako mwenyewe. Unahitaji kijikana nafsi yako kuwa kuna chaguo moja tu kwenye kile ulichopanga kufanya, nacho ni matokeo na sio sababu. Katika kufanikiwa kuijenga nidhamu binafsi UVUMILIVU ni kiungo muhimu sana.

**Nidhamu ya muda.** Muda ni mali. Muda ni fedha. Hii ni misemo inayoashiria ni kwa namna gani muda ulivyo muhimu sana kwenye mafanikio. Utafanya chochote kama utakuwa na muda. Lakini pia mafanikio mengi yanachukua muda mrefu kutokea hivyo kadri utakavyokuwa unapoteza muda ndivyo utakavyochelewa kupata mafanikio au hata kuyakosa kabisa. Kufanikiwa ni kutumia muda kwa ufanisi mkubwa. Hii inawezekana na kujenga nidhamu kali ya muda. Huwezi kutunza muda bali kuutumia vizuri.

**Nidhamu ya fedha.** Fedha ni neno lililokaa sana akilini mwa watu wengi. Jitihada nyingi zinazofanywa na binadamu zinalenga kupata fedha. Hii ni kwasababu fedha inatatua changamoto nyingi. Utakuwa na uhuru mkubwa kama utakuwa na fedha za kutosha. Licha ya watu kuwa na uhitaji mkubwa wa fedha, lakini imekuwa siyo rahisi kuwa na fedha nyingi za kukupa uhuru. Unahitaji msukumo mkubwa wa kuchukua hatua ulizoziweka kwa ajili ya

kuzalisha, kuweka na kuthibiti fedha. Hii ni nidhamu muhimu unayotakiwa kuijenga.

**Nidhamu ya kazi.** Kuna rafiki mmoja ambaye ukiambatana naye kwenye safari ya kuyafikia mafanikio hatakuacha kamwe. Ni mwaminifu sana. Bahati mbaya ni rafiki ambaye huwezi kumwepuka kama kweli unataka matokeo. Rafiki huyu ni kazi. Hakuna mbadala wa kazi. Hakuna matokeo yoyote bila kazi.

Pia kazi hutangulia mafanikio, hujaweka kazi usitegemee mafanikio yoyote. Watu wengi wamekuwa wakikwepa kazi huku wakiamini kuwa watafanikiwa bila kazi. Mwili wako kwa asili ni mvivu. Unahitaji msukumo mkubwa kutoka ndani yako ili kuweza kuweka kazi katika mipango yako kisha kupata matokeo. Hapa ndipo kitabu hiki kitakapokusaidia wewe kujenga nidhamu kali ya kazi ili uweze kupata mafanikio.

**Toa matokeo siyo sababu.** Kwa sababu kazi ndiyo inayotoa matokeo na watu hawapendi kuweka kazi kwa sababu ya maumivu, hivyo hutafuta sehemu ya kukimbilia. Kimbilio pekee huwa ni kutoa sababu kwa nini hawawezi kufanya kazi. Hiki ndicho kilichowaponza watu wengi walioshindwa.

Wana utajiri wa sababu za kwa nini wameshindwa kuchukua hatua badala ya utajiri wa matokeo ya kuwapa mafanikio. Utafanya nini ili utoe matokeo na sio sababu? Kitabu hiki kitakupa mwongozo wa kujenga nidhamu itakayokusaidi kujisukuma kuchukua hatua kisha kupata matokeo badala ya kukimbilia kutoa sababu.

Ili nidhamu iwe msaada katika maisha yako, inapaswa lisiwe tukio bali sehemu ya maisha yako. Hivyo ili kufanikiwa kujenga nidhamu ya kudumu huna budi kuifanya kuwa tabia yako. Utafanikiwa hilo kama utaifanya kuwa sehemu ya maisha yako. Kwamfano ili kuwa na afya njema, weka kufanya mazeozi kila siku kama sehemu ya maisha yako. Kitabu hiki kitakusaidia namna ya kuifanya nidhamu kuwa tabia.

Ndugu ndoto zako zitatimia, kusudi lako utaliishi kikamilifu na utatimiza malengo yako kama utafanikiwa kujenga tabia hii muhimu ya nidhamu maishani mwako. Hii ndiyo itakayokusaidia kuamsha nguvu kubwa iliyolala ndani yako ya kufanya mambo makubwa. Kitabu hiki ni mwongozo sahihi wa kukusaidia kujenga nidhamu kali muhimu katika maisha yako. Kisome na chukua hatua zilizopendekezwa kwenye kila mwisho wa sura. Hakika mafanikio yatakuwa upande wako.

Nakutakia kila la kheri.
Alfred Mwanyika